PHISH ALERT BUTTON

KnowBe4
Human error. Conquered.

Kitufe cha Phish Alert Button (PAB) hukuruhusu uripoti barua pepe unazoshuku ili shirika lako liweze kuwalinda wafanyakazi kama wewe! Tumia maelezo yaliyo hapa chini ili ufahamu ni wakati gani unafaa kutumia kitufe cha PAB, jinsi ya kutofautisha kati ya barua taka na barua pepe za wizi wa data binafsi na jinsi ya kuripoti barua pepe unazoshuku.

LINI?

Tumia Kitufe cha Phish Alert Button (PAB) unaposhuku kwamba umepokea barua pepe ya wizi wa data binafsi. PAB hutumiwa kuripoti barua pepe unazoamini kuwa ni zenye nia mbaya.

KWA NINI?

Kuripoti barua pepe kutakusaidia wewe na shirika lako kuwa salama zaidi. Ukiripoti barua pepe, barua pepe hatarishi huondolewa kwenye kikasha chako na shirika lako hufahamishwa kuhusu uwezekano wa kuathirika. Shirika lako likishajua kuhusu uwezekano huu wa kuathiriwa, linaweza kujilinda ipasavyo dhidi ya vitisho hivyo. Una umuhimu katika mchakato wa kuhakikisha kuwa shirika lako halishambuliwi na wahalifu wa mtandaoni.

NINI?

Ili ujue ni barua pepe zipi unafaa kuripoti, ni vyema ujue tofauti kati ya barua taka na barua pepe zenye lengo baya la kuiba data ya binafsi. Epuka kuripoti barua taka kwa sababu kufanya hivyo kunaweza kuzuia timu ya Teknolojia ya Habari katika shirika lako kutambua barua pepe za wizi wa data binafsi kwa wakati.

Tumia jedwali lililo hapa chini kufahamu tofauti kati ya barua taka na barua pepe za wizi wa data binafsi:

WIZI WA DATA BINAFSI	BARUA TAKA
Barua pepe za wizi wa data binafsi hutumwa na wahalifu wa mtandaoni kwa lengo la kukushawishi ubofye kiungo au uwape taarifa fulani nyeti au ya binafsi.	Kwa kawaida barua taka hutumwa na kampuni zinazojaribu kukuuzia bidhaa au huduma.
Huwa na dhana ya kuwa ya dharura (“chukua hatua sasa!”)	Barua pepe “taka” ambayo hujaomba au usiyohitaji
Hukuomba taarifa nyeti kama vile, majina unayotumia kuingia kwenye akaunti, manenosiri, au taarifa za kadi ya mikopo	Barua pepe zinazotumwa ili kutangaza bidhaa
Inaweza kuwa ya binafsi zaidi au inayokulenga wewe au shirika lako kimahususi	Barua pepe kama vile msururu wa barua zinazosambazwa, kuponi, maombi ya mchango na majarida usiyohitaji

VIPI?

Sasa kwa vile umejua tofauti kati ya barua za wizi wa data binafsi na barua taka, hivi ndivyo unavyoweza kufanya ili kuripoti barua pepe unazoshuku kwa kutumia PAB.

1. Huku ukiwa umefungua barua pepe yoyote, bofya aikoni ya PAB.
2. Ukiona arifa inayokuuliza kama unataka kuripoti barua pepe, bofya **Ndiyo** ili uthibitishe hatua unayochukua.
3. Utaona ujumbe ukithibitisha kwamba umefanikiwa kuripoti barua pepe.

HATIMAYE...

Kumbuka “Kusita, Kuangalia, na Kufikiria!” kabla ya kubofya.

© 2023 KnowBe4, Inc.